# KUKATA MANENO

## Nguvu ya Maamuzi na Uthubutu



Pastor James Kalekwa

# KUKATA MANENO:

*Nguvu ya Maamuzi na Uthubutu.*

James Kalekwa

# Orodha ya Yaliyomo

**Tabaruku** ........................................ 4

**Salamu na Utangulizi** ........................................ 5

**SURA YA KWANZA:** ........................................ 7

**DHANA YA MAAMUZI NA UTHUBUTU** ........................................ 7

SURA YA PILI: ........................................ 13

SIFA ZA MAAMUZI ........................................ 13

**SURA YA TATU:** ........................................ 20

**MIFANO YA MAAMUZI** ........................................ 20

**Kuhusu Mwandishi:** ........................................ 38

**Kuhusu New Vine Church:** ........................................ 38

**Mawasiliano na Mwandishi:** ........................................ 40

## Tabaruku

Mfululizo wa vitabu hivi vya kieltroniki (e-books) bure kwa kila atakaye; ni himizo la kiungu ndani yangu kuujaza ulimwengu kwa maarifa ya utukufu wa Mungu kama maji yaifunikavyo bahari.

Ninatabaruku kitabu hiki kwa kanisa la Kristo na kwa nchi yangu niipendayo, Tanzania.

Kanisa litashinda na kushamiri zaidi!

Tanzania, ninakupenda kwa moyo wote!

## Salamu na Utangulizi

Mfululizo huu wa vitabu vya kieletroniki ni maono ambayo Mungu ameweka ndani ya mtumishi wake, mume wangu mpenzi, kama namna yake ya kuonyesha shukurani kwa Mungu kwa zawadi ya maisha.

Ninamfahamu mume wangu kama mtu anayempenda Mungu kupitiliza. Yuko tayari kulipia gharama yoyote ile kuonyesha hilo. Ni mtu anayewapenda watu wa Mungu kwa namna ambayo sijawahi kuona. Yamekuwa ni maombi yake kuyagusa maisha ya wengi kwa kadiri inavyowezekana kabla Yesu Kristo hajarudi.

Anapoadhimisha siku ya kuzaliwa kwake **Juni 20**, amekuandikia kitabu hiki, akapangilia na kufanya kipatikane kwako bila malipo yoyote. Nimemwona anavyokesha; wakati mwingine kuamka alfajiri sana au kuchelewa sana kulala ili kukamilisha uandishi. Nimemuona anavyoomba na kuombea wasomaji, anavyojisomea na kutafiti ili kuhakikisha anafanya uwasilishaji wa thamani.

Ningependa tuthamini zawadi hii ambayo sisi wengine tunanufaika nayo bila kulipia gharama:

1. Mshukuru Mungu pamoja nasi kwa zawadi hii ya maisha ya Pastor James Kalekwa kisha muombee maisha marefu na afya njema.
2. Mwandikie ujumbe wa kumsalimu na kumpongeza ukisema ni kwa namna gani

huduma yake imeyagusa maisha yako. Ninajua hili litaufurahisha sana moyo wake.

3. Wafikishie vitabu hivi walau watu hamsini tu. Ni vitabu vinatolewa bila malipo (vimeyagharimu maisha ya mwandishi ili vikufikie).
4. Usiuze vitabu hivi. Tuligundua kuwa kuna watu wanavisambaza kwa malipo ya fedha. Hiyo si sawa. Itakuwa ni kwa hasara yako mwenyewe ukifanya hivyo.

Baada ya kuyasema hayo, nikuhakikishie ya kwamba mtu huyu mkuu wa Mungu amejaa hekima za kiungu na neno ambalo siku zote hutokeza shuhuda maishani mwa wengi. Kwa kusoma kitabu hiki, ushuhuda wako unafuatia. Nikutakie usomaji mwema.

Na heri ya kuzaliwa kwa mpendwa wetu, zawadi ya mbingu kwenye kizazi chetu, Pastor JK.

Frida James Kalekwa (Mama Pastor JK)
Mke wa mwandishi
Juni, 2024
Dodoma, Tanzania

# SURA YA KWANZA:

# DHANA YA MAAMUZI NA UTHUBUTU

Maisha ya mwanadamu yamejawa na machaguo, maisha ya mwanadamu ni mfululizo wa maamuzi, maamuzi ni pumzi, huwezi kuishi bila kufanya maamuzi, ni wafu tu ndiyo ambao hawako tena kwenye nafasi ya kufanya maamuzi. Na kwa kuwa wewe sio mfu kitabu hiki kitakujengea uwezo na kukupa nguvu ili uishi na kuwa mtu wa matokeo, kwa kitabu hiki nakutarajia utakuwa mtu anayefanya maamuzi.

Kuna aina mbalimbali za nguvu, kuna nguvu ya Roho Mtakatifu (upako), nguvu ya imani, hekima, fedha, maono, jina jema, baraka, maongozi ya kiungu na nguvu ya kufululiza, na nguvu ya maamuzi na uthubutu.


Uthubutu na Maamuzi ni nguvu itakayokufanya kuwa mtu wa matokeo.

Yoel 3:14 *“Makutano makubwa, makutano makubwa, wamo katika bonde la kukata maneno! Kwa maana siku ya BWANA i karibu, katika bonde la kukata maneno.”*

Siku ya BWANA ni siku ya mwisho, siku Yesu atakayorudi, na bonde la kukata maneno ni maisha kabla ya siku hiyo, kabla ya ng’ambo ya pili kuna bonde la kukata maneno.

a) Bonde la kukata maneno

Haya Maisha/ hii dunia tuliyopo ndiyo Yoeli anaita bonde la kukata maneno. Kama mwalimu, nitatumia taswira kusaidia uelewa wako kwenye eneo hili.




Taswira iliyoambatanishwa hapo juu inaonyesha juu ya “aina mbili” za milele (Kimsingi hakuna milele mbili la sivyo itapoteza sifa ya milele). Nimefikiria mfano huu ili kulielewa bonde la kukata maneno.

Kabla wewe hujazaliwa neno la Mungu linaonyesha alikufahamu. Maana yake ulikuwepo. Ulikuwepo kwenye mfumo gani na mwonekano gani… huo ni mjadala mwingine.

*“Neno la BWANA lilinijia, kusema, **Kabla sijakuumba katika tumbo nalikujua, na kabla hujatoka tumboni, nalikutakasa**; nimekuweka kuwa nabii wa mataifa.”* Yeremia 1:4-5

Lakini ni nani kati yetu aliyefanya maamuzi ya kuzaliwa kwake – wazazi, nyakati, taifa, namna ya kuzaliwa na mambo yanayofanana na hayo. Hakuna aliyefanya maamuzi kwenye milele iliyopita. Hakuna chumba cha maamuzi.

Kuhusu milele ijayo nako huko hakuna maamuzi binafsi. Maisha yamepangiliwa na kuratibiwa.

Sehemu pekee aliyonayo mwanadamu ni katikati ya milele iliyopita na milele ijayo. Hapo ndipo penye bonde la kukata maneno.

b) Kukata maneno

Yoeli anaeleza kuwa kwenye bonde hili la kukata maneno kuna kusanyiko kubwa/mkutano mkubwa yaani idadi kubwa ya watu. Jina la eneo linapendekeza shughuli inayoendela kwenye eno husika. Panaitwa Bonde la Kukata Maneno maana yake shughuli inayoendela ni KUKATA MANENO. Kila sekunde iendayo kwa Mungu, kuna maamuzi mabilioni yanafanyika hapa duniani.

MAANA YA KUKATA MANENO

Mit 16:10 *"Kukata maneno huwa katika midomo ya mfalme; Kinywa chake hakitakosa katika hukumu."*

Mwandishi wa Mithali anaonyesha kukata maneno kuwa ni kufanya hukumu au maamuzi au suluhisho.

1 kor 6:5 *"Nasema hayo nipate kuwatahayarisha. Je! Ndivyo, kwamba kwenu hakuna hata mtu mmoja mwenye hekima, awezaye kukata maneno ya ndugu zake?"*

Mtume Paulo anaonyesha kuwa kukata maneno kupo ndani ya uwezo wa wenye hekima tu.

Mdo 24:22 *"Basi Feliki aliwaahirisha, kwa sababu alijua habari za Njia ile kwa usahihi zaidi, akasema, Lisia jemadari atakapotelemka nitakata maneno yenu."*

i. Ni kufanya maamuzi, ni kufikia hitimisho
ii. Ni kufikia ukomo.
iii. Kuchagua uelekeo kutokana na hoja kadhaa
iv. Kufanya uchaguzi

Kwa msingi huo Yoeli anaonyesha kuwa wanadamu wote wapo kwenye bonde la kukata maneno (yaani kuamua, kuchagua, kufikia ukomo wa hoja), ni kweli kabla ya kusoma kitabu hiki umekata maneno kati ya kusoma au kutokukisoma. Mwanadamu anakabiliwa na maamuzi siku kwa siku kwenye kila jambo kiasi kwamba anachukulia kawaida.

Kuna umuhimu wa kuzingatia unapofanya maamuzi.

Maisha yamejawa na machaguo mengi, mfano vijana wengi wanakabiliwa na kuchagua mwenzi wa Maisha, unaweza kujiuliza kwanini hauendi tu kuchukua mtu yeyote kuwa mwenzi wako. Una nguo nyingi, una usafiri

mwingi n.k huwezi kufanya yote kwa wakati mmoja, lazima uchague. Maisha yamejaa machaguo.

Maisha yamejaa maamuzi, yamejaa njia panda, kila mara utafikia wakati ambao unapaswa uchague.

Ukweli kuhusu maamuzi ni kuwa, unapochagua jambo moja kwenye mengi kwenda nalo unakuwa umechaguua kutoenda na mambo mengine yote.

# SURA YA PILI:

# SIFA ZA MAAMUZI

i. Ulazima

Kwamba ufanye maamuzi au usifanye? Hauna tena hiyo hiyari kwenye bonde hili. Maamuzi ni lazima, huwezi kuyakwepa wala huwezi kuyakimbia, na kwanza kutokuchagua kuamua unakuwa umechagua pia. Kila sekunde unakabiliwa na maamuzi – uamke au uendelee kulala? Usitishe uhai wako au uendelee kuishi? Ulipe gharama za ukuu au uendelee kuwa mtu wa wastani? Uyaishi maisha kwa kukusudia (being intentional) au uishi kama vile ni ajali? Ni lazima ufanye maamuzi!

i. Ni Binafsi

Huwezi kukasimisha maamuzi, ni lazima uamue, huwezi kumgawia mtu aamue kwa ajili na kwa niaba yako. Hata hivyo, ukiamua kukasimisha, nao ni uamuzi! Na hili limekuwa tatizo kwa vijana wengi hasa mabinti. Wengi wanategemea wazazi, marafiki kuwafanyia maamuzi, wengine hawawezi hata kuamua wavae nguo gani.

Wamekuwa kwenye hali ya utegemezi kiasi hicho. Jifunze kufanya maamuzi yako mwenyewe kwasababu mnufaika na/au mwathirika wa kwanza wa maamuzi yako ni wewe mwenyewe.

Watu wasiofanya maamuzi yao wenyewe huwa na laumu nyingi sana. Wanapenda kulaumu wengine kwa kila kitu. Hata kuwa na furaha ni maamuzi; watu tegemezi hata wasiposalimiwa tu wanakosa furaha.

ii. Ni mbegu

Kila maamuzi ni mbegu kwa maana ya kwamba yatakuzalia kitu na matokeo yake ni endelevu. Mtume Paulo anawaambia wagalatia:

*"Msidanganyike, Mungu hadhihakiwi; kwa kuwa cho chote apandacho mtu, ndicho atakachovuna."* Wagalatia 6:7

Shambani kila mkulima ni nabii; ukichukua mahindi ukapanda utavuna mahindi. Ukitaka miwa, panda miwa; huwezi kupanda maharage ukavuna mahindi. Maamuzi unayoyachukua ni mbegu, maamuzi unayoyafanya kwenye maisha yako ni mbegu, kwa lugha nyingine

kabla ya kufanya maamuzi angalia matokeo ya baadaye ili yakufikirishe sasa. Piga picha ya baadaye uone kama unaweza kuipokea na kuifurahia, kama unatabasamu kwenye hayo matokeo chukua hiyo mbegu ya maamuzi, na kama haufurahii matokeo ya hiyo mbegu achana na hayo maamuzi.

Kwa kuwa maamuzi ni mbegu hayakuathiri wewe tu, bali yanawaathiri na watu wanaokuhusu na wanaokuzunguka.

Mfano wana wa Ishamaeli wanawatesa na kuwasumbua waana wa Isaka hadi leo kwasababu ya maamuzi ya Ibrahimu.

Mimi nisingeamua kuandika hiki kitabu kisingekufikia mikononi siku ya leo. Ni maamuzi!

Nikudokeze tu siri moja muhimu sana hapa ninapomalizia kujadili kuhusu swala la maamuzi kama mbegu: Uko huru kuchagua, kujadili, kufikiri kuhusu aina ya mbegu. Hauna uhuru wowote wa kuchagua mavuno ya mbegu hiyo baada tu ya kuipanda. Yaani, unaweza ukachagua hatua ya kimaamuzi ya kuchukua.

Huna tena nafasi kuchagua matokeo ya maamuzi hayo. Matokeo yamo ndani ya maamuzi. Mavuno yamo ndani ya mbegu!

iii. Kwa kadiri ambavyo unafanya maamuzi ndivyo ambavyo makali yako ya kukata maneno yanaongezeka.

Maamuzi yanatisha kuyafanya. Maamuzi yanachosha kuyafanya. Kiasi kwamba imepelekea wengine kufanya maamuzi bila kuyafikiria tena. Habari njema ni kwamba kwa kadiri unavyoendelea kufanya maamuzi makubwa na madogo ndivyo ambavyo unazidi kuwa na uwezo mkubwa wa kufanya maamuzi. Kwa kadiri unavyozidi kufanya maamuzi kwa usahihi, ndivyo uwezo wa kufanya maamuzi sahihi unaongezeka ndani yako. Kwa kadiri unavyohusisha fikra, upembuzi na ujasiri katika kufanya maamuzi, ndivyo ambavyo makali yako ya kimaamuzi kwa njia hizo yanazidi kuimarika.

Mfano nimekuja kubaini jinsi gani ilivyo ngumu kuandika barua ya kuacha ajira kwa sababu sio maamuzi ambayo wengi wameyazoelea kufanya. Unakutana na

mtu ambaye analalamika, analia na kwa mazungumzo anaonyesha kabisa yuko tayari hata sekunde ijayo kuondoka eneo hilo la kazi lakini hawezi kuandika barua. Sasa, si kwamba hawezi kuandika kwa maana ya kuweka maandishi kwenye karatasi bali kufanya hayo maamuzi. Hata kwenye mitaala ya elimu hufundishwa kwa uchache sana namna ya kuondoka kwenye ajira. Muda mwingi tumefundishwa "namna ya kutafuta au kuomba kazi".

iv. Huwezi kuamua kuchagua pande zote mbili za maamuzi

Kuna maamuzi ambayo yana pande mbili pinzani. Huwezi kuwa na pande zote kwa wakati mmoja bila kuleta madhara. Mfano huwezi kusema unamuoa dada Frida na bado unamuelewa sana dada Winnie. Hapana! Huwezi kuwa umelala na umeamka kwa wakati huo huo; Huwezi kustawi na kufanikiwa kwa tabia za watu walioshindwa; Huwezi kuwa mwanandoa na maisha ya ubachela kwa wakti huo huo. Hapana! Huwezi kufanya hivyo, unaweza kuchagua kitu kimoja kwa muda mmoja na unapaswa kufurahia machaguo yako (Exclusivity).

v. Maamuzi huathiri maisha yetu na wanaotuhusu

Maamuzi na matokeo yake huendelea na kuwagusa watu wanaotuhusu. Matokeo ya maamuzi huishi baada yetu na kuathiri kwa uchanya au uhasi watu wetu.

*"Nazishuhudiza mbingu na nchi juu yenu hivi leo, kuwa nimekuwekea mbele yako uzima na mauti, baraka na laana;* ***basi chagua uzima, ili uwe hai, wewe na uzao wako****;"* Kumbukumbu la Torati 30:19

*"Tena yaweza kusemwa ya kuwa,* ***kwa njia ya Ibrahimu, hata Lawi apokeaye sehemu ya kumi alitoa sehemu ya kumi;****"* Waebrania 7:9

*"Usivisujudie wala kuvitumikia; kwa kuwa mimi, BWANA, Mungu wako, ni Mungu mwenye wivu;* ***nawapatiliza wana maovu ya baba zao, hata kizazi cha tatu na cha nne cha wanichukiao, nami nawarehemu***

***maelfu elfu wanipendao, na kuzishika amri zangu****.”*
Kutoka 20:5-6

*“Kwa hiyo,* ***kama kwa mtu mmoja dhambi iliingia ulimwenguni****, na kwa dhambi hiyo mauti; na* ***hivyo mauti ikawafikia watu*** *wote kwa sababu wote wamefanya dhambi;”* Warumi 5:12

Hii ikuamshe kiufahamu ya kwamba hata kwa maamuzi unayoyafanya sirini, watu wanaokuhusu watayavuna hadharani. Unapaswa kuamua vyema!

Kwa mfano, maamuzi afanyayo mtu kuhusiana na maswala ya kingono (sexuality) huwagusa mpaka watoto wake ambao inawezekana hawapo muda huo. Ukiamua kuzaa watoto kabla ya ndoa, huwezi kuzuilia matokeo yanayokuja na maamuzi hayo kwa watoto. Ukiamua kuzaa nje ya ndoa, kuna matokeo pia yanakuja na kuwagusa watoto wako.

# SURA YA TATU:

# MIFANO YA MAAMUZI

Sisi ni wageni kwenye baadaye ijayo, hatujui yajayo yatakuwaje, na kwahiyo maamuzi yanaambatana na uthubutu na yanadai uthubutu. Wakati wa kufanya maamuzi kila mtu huwa ana vita ya kujiuliza *"vipi kama haitakuwa hivyo tunavyotarajia",* hii hali ipo ili kutuonyesha kuwa sisi sio wenyeji kwenye nchi.

*"**Mimi ni mgeni katika nchi,***

*Usinifiche maagizo yako."*

Zaburi 119:19

Huu ugeni unaozungumzwa hapa ni kuhusu mambo yajayo. Haujawahi kuwa kwenye wakati wako ujao. Hivyo basi, hujui kitu gani kianendelea huko. Huna uhakika ya kwamba mambo yatakuwaje huko siku za usoni. Si ajabu mzaburi alijisalimisha kwa Mungu kwa hali ya utegemezi kiasi hicho.

Hautakuwa na taarifa zote ili kufanya maamuzi; Ukiona una taarifa zote ili kufanya maamuzi ujue unazungumzia wakati uliopita na sio ujao. Jambo hili linayafanya maamuzi kuwa mtego kwa watu wengi.

Kama sisi ni wageni kwenye nchi kiasi hicho, basi kufanya maamuzi linakuwa si jambo rahisi sana. Ndiyo maana basi ninahusianisha kukata maneno na moyo wa uthubutu! Uthubutu tunaouzungumzia hapa ni zao la imani na tumaini, utafungua biashara na hujui kama watu watakuja kununua au la! Utaandika kitabu na hujui kama watu watakisoma au la! Unamwoza binti yako hujui kama anapata mume kichomi au la! Kinachotufanya kufurahia matokeo ni imani na tumaini inayoitwa uthubutu. Mtu asiyeweza kuthubutu hana imani na tumani.

Kwahiyo usikae ukafikiria itakuja kutokea siku moja utakuwa na taarifa zote mkononi mwako ndiyo ufanye maamuzi; Hiyo siku haipo, kila siku inabidi ujue Imani na tumaini vinavyozaa uthubutu ndiyo vibebe maamuzi yako.

Watu wanaofanya maamuzi na uthubutu ndiyo watu wenye matokeo, watu wasio na matokeo ni watu wasio na maamuzi na uthubutu.

Hebu ngoja nikutazamishe mifano ya kibiblia ili ikusaidie kumeng'enya jambo hili kwa urahisi.

1) WAKOMA WANNE

2 Wafalme 7:1-16

Ni habari ya njaa iliyotokea katika Israeli kiasi kwamba watu wakila watoto wao na wengine wakila mavi ya njiwa kwasababu mji wa Israeli ulikuwa umehusuriwa (umezingirwa na Jeshi la washami).

2 Fal 7:3-4 *"Basi walikuwapo watu wanne wenye ukoma, penye lango la mji;* ***wakasemezana, Mbona tunakaa hapa hata tufe? Tukisema, Tutaingia mjini, mjini mna njaa, nasi tutakufa humo; nasi tukikaa hapa, tutakufa vile vile. Haya! Twende tukaliendee jeshi la Washami; wakituhifadhi hai tutaishi; wakituua, tutakufa tu.****"*

Ninataka utazame kikao cha wakoma kuhusu hali yao. Kisha uende mbele kutazama muundo wao wa kimawazo (thought pattern). Ajenda kuu ya kikao ni NAMNA YA KUENDELEA KUISHI.

Kwa wasiofahamu, ukoma ni ugonjwa wa nasaba; ugonjwa wa kurithi. Ugonjwa huo unaweza kuwa ndani ya mtu bila kuwa na dalili zozote za nje, akawa ameubeba tu. Na kuna wale ambao walikuwa na dalili za nje za ugonjwa kama vile vodonda, vidole kukatika na hali ya mabaka. Sasa, kwenye taratibu za kiyahudi, mtu mwenye dalili za nje za ukoma aliwekwa nje ya lango ili apone na kuondokwa na dalili za nje.

*"Kisha BWANA akanena na Musa, na kumwambia, 2Waamrishe wana wa Israeli kwamba wamtoe kila mwenye ukoma maragoni, na kila mtu aliye na kisonono, na kila aliye najisi kwa ajili ya wafu; mtawatoa nje wote, waume kwa wake, mtawaweka nje ya marago; ili wasiyatie unajisi marago yao, ambayo mimi naketi katikati yake."* Hesabu 5:1-3

*“Kisha mwenye ukoma aliye na pigo ndani yake, nguo zake zitararuliwa, na nywele za kichwa chake zitaachwa wazi, naye atafunika mdomo wake wa juu, naye atapiga kelele, Ni najisi, ni najisi. Siku zote ambazo pigo li ndani yake, yeye atakuwa mwenye unajisi; yeye yu najisi; atakaa peke yake; makazi yake yatakuwa nje ya marago.”* Mambo ya Walawi 13:45-46

Sasa, ili waweze kurudi ndani ya kambi na kujumuika na wenzao walipaswa kujionyesha kwa kuhani mkuu ili aidhinishe ya kwamba sasa wanaweza kurudi mjini. Wakati wote wakiwa pembeni ya mji, ndugu zao wangekuja kuwahudumia kwa mahitaji ya muhimu kama chakula. Sivyo ilivyokuwa kwa hawa wakoma wanne. Hiyo ikapelekea kikao cha wakoma.

***wakasemezana, Mbona tunakaa hapa hata tufe? Tukisema, Tutaingia mjini, mjini mna njaa, nasi tutakufa humo; nasi tukikaa hapa, tutakufa vile vile.***


Haya ni mazungumzo mazito sana kwenye kikao. Ni maswali muhimu sana ya kujiuliza. Ni ufkiri mzuri sana wa kuufuatia.

Hatua ya kwanza ya kufanya maamuzi ni kujiuliza maswali. Huwezi kuwa na uthubutu kama utayaepuka maswali magumu. ***“Mbona tunakaa hapa mpaka tufe?”*** na baada ya hapo wanaendelea kuchambua machaguo yaliyomo mikononi mwao: Ama waende mjini, yaani, waingie kule ambako kisheria hawaruhusiwi kuingia. Walau wana taarifa ya nini kinaendela mjini – hakuna chakula. Kwa hiyo huko nako watakufa! Lakini wakiendelea kubaki hapo walipo watakufa… umeelewa sasa kwa nini nimesema ajenda kuu ya kikao ni namna ya kuendelea kuishi? Angalia neno kufa linavyojirudia rudia kwenye sentensi zao. Linapendekeza wazo kuu. Hawataki kufa kwa njaa.

***Haya! Twende tukaliendee jeshi la Washami; wakituhifadhi hai tutaishi; wakituua, tutakufa tu.***

Kufanya maamuzi ni kutazama mbele na kujiuliza nini kitakuwa vipi. Utaona wakoma wanachagua kwenda kwenye jeshi la washami ambako walau kuna uwezekano wa kupata chakula. Ninamwamini Roho Mtakatifu hili halitakupita. Ngoja nikuwekee hapa kwa

urahisi zaidi. Kwenye machaguo ya wakoma kulikuwa na maeneo matatu ya kuyaendea:




Sehemu pekee ambao kulikuwa kuna mwanya ni kwenye kambi ya Washami- kulikuwa na chakula. Kimsingi, hilo ndilo hitaji lao. Wakoma wakaamini pia kuna uwezekano wa kuhifadhiwa hai na Washami… ndiyo kuna uwezekano wa kufa pia. Hata hivyo, kufa ni kibwagizo sasa kwao. Ni *"common denominator"*. Chaguo pekee ni kwenda kufa kilipo chakula. Ndiyo maana unaona kuna neno dogo linaongezeka hapa…

***“Tutakufa tu!”*** Hiyo “tu” haikuwepo wakati wanajadili yale maeneo mawili. Kuna ujumbe mkubwa sana humo.

Wakaona ni heri kwenda mahali penye uwezekano wa kuhifadhiwa na kuishi kuliko kwenda au kubaki kwenye njaa ambako unakufa mwenyewe.

Kabla ya kufanya maamuzi jambo la kwanza jiulize kwanini nibaki hapa, kwanini nibaki kwenye hali niliyonayo, kisha jiulize natokaje hapa?

*“Basi wakaondoka kabla ya mapambazuko, ili waende mpaka kituo cha Washami; na walipofika mwanzo wa kimo cha Washami,* ***kumbe! Hapana mtu****.* ***Kwa maana Bwana alikuwa amewasikizisha Washami kishindo cha miendo ya magari, na kishindo cha farasi, kama kishindo cha jeshi kubwa; wakaambiana****, Tazama, mfalme wa Israeli amewaajiri wafalme wa Wahiti, na wafalme wa Wamisri, waje wapigane nasi.* ***Kwa hiyo wakaondoka, wakakimbia kungali giza bado, wakaziacha hema zao, na farasi zao, na punda zao, na kimo chao vile vile kama kilivyokuwa, wakakimbia wapate kujiponya nafsi zao.****”* 2 Fal. 7:5-7

Nimekuonyesha hapo awali ya kwamba maamuzi ni jambo hatari ndiyo maana yanadai uthubutu. Sasa, hawa ndugu baada ya kikao maazimio ikawa ni kwenda kwenye kambi ya Washami… Biblia inasema "KUMBE!" Maana yake ni *"supriiiiiiiiise"* wakakutana na mshangao wa maisha yao. Hao washami wenyewe, hawapo!

Biblia inatusimulia nyuma ya pazia nini kiliendelea. Kitu ambacho wakoma hawakijui na washami hawakijui… sisi tu tumepewa neema ya kuona pande zote kisha kuona nyuma ya pazia.

Kumbe wakoma wanne wakati wanatembea, washami walisikia: ***Kwa maana Bwana alikuwa amewasikizisha Washami kishindo cha miendo ya magari, na kishindo cha farasi, kama kishindo cha jeshi kubwa;***

Usisahau… wakoma hawajui kinachoendela nyuma ya pazia, na washami hawajui! Sasa, ni muda wa tendo la Bwana mwenyewe.

Na tunaona BWANA alitenda kutokea kwenye maamuzi yao, kama wasingaliamua kwenda wasingepata chakula.

Bwana anaongeza mvumo wa miguu yako kuelekea maamuzi yako, fanya maamuzi na uende mbele.

Maamuzi unapoyachukua Bwana ana tabia ya kuingilia kati na kubariki. Bwana anasema atabariki kazi ya mikono yako, kwahiyo acha kuchagua kazi, kinachokupa faida sio kazi ni baraka inayoachiliwa kwenye kazi yako.

Anza kufanya hatua yako, wewe ni mbarikiwa haijalishi unafanya nini baraka zako zinakufuata na zitakupata na kukuinua, chukua maamuzi, ni kuuza karanga, ni kushona viatu n.k, nenda mbele. Teknolojia ya kusikizisha kishindo cha farasi na miendo ya magari mwachie Bwana mwenyewe.

Wengi sana wanamsubiri Bwana afanye, lakini ukweli ni kuwa Bwana anawasubiri sana wafanye maamuzi, kwa maana usipofanya Bwana hafanyi. Kwanza, Bwana kashafanya vitu vyote, ni wewe unasubiriwa kufanya maamuzi.

2 Fal 7:10 *"Basi wakaenda, wakawaita mabawabu wa mji; wakawaambia, Tulifika kituo cha Washami, na tazama, hapana mtu ye yote huko, wala sauti ya mtu, ila*

*farasi wamefungwa, na punda wamefungwa, na hema zao kama walivyoziacha."*

Muujiza mwingine usiosemwa sana ni huu hapa: usisahau wakati huo wakoma hawakuruhusiwa kujichanganya na watu wengine kwa maana wakoma walihesabiwa kuwa najisi na wanavyovigusa kuwa najisi. Lakini wanafanya maamuzi magumu ya kwenda mjini na kuwapasha habari watu wa mji bila kujali uwezekano wa kupigwa mawe kwa kuwa wao ni wakoma. Lakini wakachukua hatua ya kwenda na kutoa taarifa, hii inadhihirisha ukomavu wa uwezo wao wa kufanya maamuzi, kwa maana hapo awali walipofanya maamuzi magumu ya kuiendea kambi ya washami, Bwana alifanya njia. Basi, sasa hivi hawatashindwa kufanya maamuzi magumu zaidi.

Kila unapofanya maamuzi makali yako ya kufanya maamuzi yanaongezeka zaidi, thubutu zaidi, taka zaidi, amua zaidi.

Nani katika Israeli angetarajia wakoma walete habari njema namna hii? Wawe jawabu la tatizo kubwa la kitaifa? Nani alitarajia!?

2 Fal 7:12 *“Mfalme akaondoka usiku, akawaambia watumishi wake, Sasa nitawaonyesha ninyi walivyotutendea Washami. Wanajua ya kuwa tuna njaa; basi wametoka kituoni, ili kujificha kondeni, wakisema Watakapotoka mjini, tutawakamata hai; tena tutapata kuingia mjini.”*

Kati ya mfalme na wakoma ni nani anapaswa kuwa jasiri kwenye maamuzi? Unaona ni kwa jinsi gani mfalme ameathiriwa na hali kiasi kwamba haamini tena mlango wa chakula ambao Bwana ameufungua? Tunaona tena mfalme naye anabidi kufanya maamuzi ya kwenda au kutokwenda, na mwisho baada ya kupeleleza wanaenda na kuteka nyara na neno la kinabii linatimia.

*“Elisha akasema, Lisikieni neno la BWANA; BWANA asema hivi, Kesho panapo saa hii, kipimo cha unga*

*mzuri kitauzwa kwa shekeli, na vipimo viwili vya shayiri kwa shekeli, langoni pa Samaria."* 2 Fal. 7:1

Kwahiyo hata kama mtumishi wa Mungu atatamka kwako unabii, hautatokea kama hautachukua hatua, unabii unatimilizwa na maamuzi, neno la Mungu limekwisha sema, unatakiwa ufanye maamuzi sasa kupokea utimilifu wa neno la Mungu ulilopokea. Maamuzi ya namna hii ni kukubaliana na kweli ya neno la Mungu. Ni kutenda kwa utii kulielekea neno la Mungu hata kama mazingira yote hayaruhusu.

Mungu anaheshimu maamuzi, unapofanya maamuzi Mungu atasikilizisha kishindo chako.

Usisahau, neno la Mungu limeachiliwa tayari hewani. Linangojea mtu mmoja mwenye uwezo wa kufanya maamuzi na uthubutu toshelevu wa kuchukua hatua za utekelezaji.

Ninatabiri ujasiri uinuke ndani yako.

Ninatabiri uthubutu uzaliwe ndani yako.

Ninatamka uwezo uinuke ndani yako.

b. Mwanamke aliyetokwa na damu miaka 12

Mt 9:20-22 *"Na tazama, mwanamke aliyekuwa na ugonjwa wa kutoka damu muda wa miaka kumi na miwili, alikuja kwa nyuma, akaugusa upindo wa vazi lake. Kwa maana alisema moyoni mwake, Nikigusa tu upindo wa vazi lake nitapona. Yesu akageuka, akamwona, akamwambia, Jipe moyo mkuu, binti yangu; imani yako imekuponya. Yule mwanamke akapona tangu saa ile."*

Ili uweze kuthamini funzo tulalolipata kwa mama huyu aliyetokwa na damu kwa muda wa miaka kumi na miwili ni vyema ukaijua theolojia ya usafi (purity) ya Agano la Kale. Ukisoma kitabu cha Mambo ya Walawi 15 kinafafanusha kwa upana kuhusu swala hili. Kwa mwanamke aliyekuwa kwenye siku zake, alipaswa kuwa mbali na jamii yake kwa siku saba na chochote na yeyote aliyemgusa alikuwa najisi. Kuna taratibu za kufanya ili kurejeshwa kwenye jamii.

Kwa mwanamke aliyetokwa na damu (Biblia inatumia neno kitu chochote kutoka ndani ya mwili wake) zaidi ya

muda wa kawaida ya mwanamke, huyo alikuwa najisi kwa muda wote huo. Ngoja tuweke andiko hapa ujisomee mwenyewe:

*"Na mwanamke kama akitokwa na damu yake siku nyingi, nayo si katika majira ya kutengwa kwake, au kama anatoka damu kuzidi majira ya kutengwa kwake;* ***siku hizo zote za kutoka damu ya unajisi wake, atakuwa kama alivyokuwa katika siku za kutengwa kwake; yeye yu najisi****.* ***Kila kitanda akilaliacho*** *katika siku zote za kutoka damu kitakuwa kama kitanda cha kutengwa kwake;* ***na kila kitu atakachokilalia kitakuwa najisi****, kama unajisi wa kutengwa kwake.* ***Na mtu ye yote atakayevigusa vitu vile atakuwa najisi****, naye atazifua nguo zake, na kuoga majini, naye atakuwa najisi hata jioni."* Mambo ya Walawi 15:25-27

Baada ya kuelewa muktadha, sasa rudi tumtazame huyu mama najisi kwa miaka kumi na mbili mfululizo. Akibaki hapo alipo, ataendelea kuwa najisi. Akitoka aingie mjini kukutana na Yesu atapigwa mawe na atakaowagusa watakuwa najisi kwa hiyo watu

hawatataka kugusana naye na chochote kilicho kwenye mwili wake.

Hebu fikiri pamoja nami kuhusu huyu mwanamke, tengeneza taswira mawazoni mwako: Huyu mama amepoteza damu toka mwilini mwake muda wote huo… atakuwa dhaifu, ngozi yake imepauka, huenda anatembea kwa kupepesuka, kwa haraka ni ananuka, mchafu... Ninafikiri anatoa harufu ambayo huwezi kuipotezea. Ninadhani ana mwonekano ambao huwezi kuupotezea! Anatambulikana kabisa kwa kumuona… ukimuona tu unajua huyu ndiyo yule ***"Bibi najisi"***!

Paoja na hayo yote anaamua kuchukua maamuzi ya kwenda kuchukua uponyaji wake kwa Bwana Yesu akiwa anajua matokeo ya kusogea kwa watu wanaomuona kama najisi. Hakujali tena mwonekano wake utasababisha ajulikane… harufu yake itamuumbua.

Alijua wazi, amekuwa kwenye hali hiyo kwa miaka mingi. Ameichoka hali hiyo kiasi kwamba yuko tayari kujihatarishia maisha yake huku akiuendea muujiza wake.

Lengo alilokuwa nalo moyoni mwake ni hili: *"Kwa maana alisema moyoni mwake, Nikigusa tu upindo wa vazi lake nitapona."*

Ninapenda sana mwitikio wa Bwana Yesu:

*"Yesu akageuka, akamwona, akamwambia,* ***Jipe moyo mkuu, binti yangu; imani yako imekuponya****. Yule mwanamke akapona tangu saa ile."*

Alimuelewa na alimtibitishia ya kwamba ulichokifuata, umekipata! Hivi unajua Yesu yuko zaidi ya tayari? Anasubiri uthubutu wako… uchoke hiyo hali uliyo nayo kiasi chakuchukua hatua.

Ninaomba kusema ukiri wangu hapa hadharani. Huwa ninapenda kuisoma na kuielewa miujiza ya Bwana Yesu zaidi kutokea kwenye injili ya Luka. Sababu yangu ni kwamba huyu ni daktari kwa hiyo kuna namna yake ya kuelewa na kuelezea mambo ya kiafya. Hebu tuutazame muujiza huu kutokea huko na nitapenda kama ukifungua jicho lako vya kutosha kusoma taarifa za zaidi kutokakwa daktari:

Luka 8: 43-48“Na mwanamke mmoja, ambaye ametokwa na damu muda wa miaka kumi na miwili, *[aliyekuwa amegharimiwa mali zake zote kwa kuwapa waganga]* asipate kuponywa na mtu ye yote, alikwenda nyuma yake, akaugusa upindo wa vazi lake; na mara hiyo kutoka damu kwake kulikoma. Yesu akasema, Ni nani aliyenigusa? Basi, watu wote walipokana, Petro alimwambia, Bwana mkubwa, makutano haya wanakuzunguka na kukusonga. *Yesu akasema, Mtu alinigusa, maana naona ya kuwa nguvu zimenitoka*. *Yule mwanamke, alipoona ya kwamba hawezi kusitirika akaja akitetemeka, akaanguka mbele yake, akamweleza mbele ya watu wote sababu yake ya kumgusa, na jinsi alivyoponywa mara.* Akamwambia Binti, imani yako imekuponya; enenda zako na amani.”

Umegundua maamuzi ambayo yana hatari zaidi yanalipa zaidi. Na tunafahamu baada ya kufanya alichokusudia kufanya kwenye maamuzi yake akapokea muujiza wake. Ndiyo historia yake ilibadilikia hapo. Hamuwezi tena kumuita najisi!

Watu wanaweza kudharau maamuzi uliyofanya lakini matokeo ya maamuzi hayana mabishano. Kila mtu huyafurahia matokeo. Wanaweza kudharau maamuzi yako ya kumtumikia Bwana kwa mfano, lakini hawatadharau matokeo yako ya kufanya kazi ya Bwana.

**Kuhusu Mwandishi:**
Mwandishi wa kitabu hiki, James Kalekwa, ni mfuasi wa Yesu Kristo; mtoto wa kiroho wa Mchungaji Goodluck na Ziada Kyara; Mume mpenzi wa Frida, baba anayewajibika wa Joshua-Vision, Charis "Tai", Victor na Priscilla; na anafurahia kuwa mchungaji mkazi wa kanisa la New Vine jijini Dodoma.

Mchungaji James ameitwa *"Kuujaza ulimwengu kwa maarifa ya utukufu wa Mungu kama maji yaifunikavyo bahari."* [Habakuki 2:14]

**Kuhusu New Vine Church:**
Kanisa la New Vine limebeba utume wa kuinua kizazi cha kiungu kitakacholeta mguso chanya kwenye kila nyanja ya maisha kwenye jamii, taifa na mataifa. (Mathayo 5:13-14/Yoeli 2:2-11)

Makao makuu ya kanisa (Gloryland) yako Mwanza chini ya mwangalizi ambaye pia ni muasisi, Mchungaji Goodluck & Mama Ziada Kyara.

Kufahamu zaidi kuhusu kanisa hili kwa ujumla tembelea: https://www.newvinechurch.or.tz

**Mawasiliano na Mwandishi:**



NEW VINE CHURCH | Dodoma



New Vine Church limebeba utume wa kuinua kizazi cha kiungu kitacholeta mguso chanya kwenye kila nyanja ya maisha kwenye jamii, taifa na mataifa *(Mathayo 5:13 -14/Yoeli 2:2 - 11).*

Makao makuu ya kanisa (Gloryland) yako Mwanza chini ya mwangalizi ambaye pia ni muasisi, Mchungaji Goodluck & Mama Ziada Kyara.

Kufahamu zaidi kuhusu kanisa hili kwa ujumla tembelea: https://www.newvinechurch.or.tz



**Mahali tulipo:** Swaswa mkabala na geti la Waziri Mkuu, Dodoma mjini.

**Ratiba za Ibada**

**Alhamisi** Saa 11:15 jioni - saa 12:15 jioni
**Jumapili** Saa 3:00 asubuhi - saa 6:30 mchana

nvc_dodoma +255 754 917 764

# KUHUSU MWANDISHI



James Kalekwa ni amemwamini Yesu kuwa BWANA na Mwokozi wa maisha yake. Ni mtoto wa kiroho wa Mchungaji Goodluck na Ziada Kyara; ni mume mpenzi wa Frida; baba anayewajibika kwa Joshua-Vision, Charis "Tai", Victor na Priscilla. Ni mchungaji wa New Vine Church - Dodoma


pastorjameskalekwa

+255 754 917 764

pastorjameskalekwa

pastorjameskalekwa

pastorjameskalekwa

pastorjameskalekwa

MchungajiJK

+255 754 917 764